



## HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

S.L.P. 83, KALIUA, Simu Na: 0736 204 192,  
Nukushi: 0732 988 451, Barua pepe: [ded@kaliuadc.go.tz](mailto:ded@kaliuadc.go.tz),  
Tovuti: [www.kaliuadc.go.tz](http://www.kaliuadc.go.tz)

KDC/M.2/VOL.II/0056/23

03/10/2017

### TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kuzingatia kibali cha ajira Mbadala chenye Kumb Na. CFC 26/205/01 "FF"/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 anawatangazia Wananchi wote nafasi za kazi kama ifuatavyo;-

#### **A. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 29)**

##### **1. Sifa za Mwombaji**

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (Form four) au Sita (Form Six) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA LEVEL 5) katika moja ya fani Zifuatazo;- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

##### **2. Kazi za kufanya**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji

- xii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato katika kijiji
- xiii. Kuandaa na kutunza rejista ya Wakazi wote wa kijiji
- xiv. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

3. Ngazi ya Mshahara ni kulingana na Viwango vya Serikali TGSB

## **B. DEREVA DARAJA LA II (LINARUDIWA)**

### **1. Sifa za Mwombaji**

Kuajiriwa wenye Cheti cha Mtihani wa Kidato cha IV, Wenye Leseni daraja la "C" ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajali, wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II.

### **2. Kazi za kufanya**

- i. Kuendesha magari ya abiria, na malori,
- ii. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitajika matengenezo,
- iii. Kufanya matengenezo madogo katika gari,
- iv. Kutunza na kuandika daftari la safari "Log book" kwa O safari zote.

3. Ngazi ya Mshahara ni kulingana na Viwango vya Serikali TGOS A


## **4. MASHARTI YA JUMLA**

- 1. Mwombaji awe raia wa Tanzania
- 2. Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- 3. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed cv).
- 4. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha moja ya rangi ya hivi karibuni (passport size).
- 5. "Testimonials", "Provisional results", hati za matokeo ya kidato cha nne na sita "Leaving Certificate" havitatumika kama uthibitisho wa kuhitimu masomo katika ngazi husika.
- 6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na mamlaka husika.

5. Maombi yatumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P.83,  
**KALIUA.**

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 06/10/2017 saa 9.30 mchana.  
(Muda wa kuwasilisha maombi umeongezwa kutoka kwenye tangazo la kazi la tarehe 15/09/2017 lenye Kumb.Na.KDC/M.2/VOL.II/0056/20.

  
Jimmy D. Nkwamu  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**KALIUA**  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KALIUA